# Mkulima na Uhakika wa Chakula

## Mwenendo wa Warsha ya Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

**Iliyofanyika Katika Kituo cha Nazareti, Njombe**

**13 -15 Novemba 2000**



[illegible] ilitayarishwa na Mradi wa

**[illegible] ula na Pato la Kaya kwa Wakulima [illegible] adogowadogo Tanzania**

[illegible] Mradi Unaotilia Mkazo Wanawake

Mradi huu upo chini ya Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili

(TARP II - SUA Project)

# Mwenendo wa Warsha ya Kuimarisha Uhusiano Baina ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

**Iliyofanyika Katika Kituo cha Nazareti, Njombe**

*13 - 15 Novemba 2000*

---

Warsha hii ilitayarishwa na

**Kamati ya Utekelezaji wa Mradi wa**

**Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania: Mradi wa Utafiti Unaotilia Mkazo Wanawake**

Mradi huu upo chini ya Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili

(TARP II – SUA Project)

***Imeandikwa na***

Bw. A. M. Bakari

***Imehaririwa na***

Kamati ya Utekelezaji wa Mradi:

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B Kinabo | Mratibu |
| Dk. (Bi.) J. Lyimo Macha | Mjumbe |
| Prof. R. Malimbwi | Mjumbe |
| Prof. E. Batamuzi | Mjumbe |
| Dk. P. Makungu | Mjumbe |
| Dk. A. J. P. Tarimo | Mjumbe |

**ISNB: 9987 605 22 2**

*Kimechapishwa na:*

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania
(TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo namba: TS 2-06

**© 2000 TARP II – SUA Project**

Picha ya Kwenye Jalada: Wakulima, watafiti na washauri wa wakulima kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa Warsha ya Wakulima iliyofanyika tarehe 13 -15 Novemba 2000. Picha inaonyesha washiriki wakitumia michoro katika kubainisha uhusiano baina ya matatizo kwa jinsi yanavyosababishana.

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway, kinatekeleza mradi huu wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD).

Matokeo yanayotarajiwa yako makuu matano, nayo ni:

1. Matokeo ya tafiti za kilimo zinazolenga matatizo ya wakulima wadogowadogo.
2. Kuimarishwa kwa uhusiano kati ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima.
3. Wahitimu 32 wa Wizara ya Kilimo wenye shahada za juu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.
4. Rasimu ya mapendekezo kwa Serikali na wahisani juu ya mfumo endelevu wa kugharamia shughuli za utafiti wa kilimo.
5. Tathmini ya mabadiliko yatokanayo na tafiti zilizokwishafanyika na zinazofanyika sasa.

Kwa hiyo kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kuimarisha uhusiano wa wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo.
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo.
3. Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi.
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

Chapisho hili linawasilisha Mwenendo wa Warsha ya Kuimarisha Uhusiano baina ya Wakulima, Watafiti, Washauri wa Wakulima iliyofanyika katika Kituo cha Nazareti Njombe tarehe 13 hadi 15 Novemba 2000. Japo warsha iliendeshwa kwa Kiswahili, Mwenendo wa Warsha umechapishwa na kutolewa kwa Kiswahili na kwa Kiingereza. Matoleo yote mawili yanafanana, isipokuwa, toleo la Kiingereza halina hotuba nzima za ufunguzi na ufungaji wa Warsha.

*L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ADP | Animal Draught Power (*Kituo cha kuendeleza matumizi ya wanyamakazi Wilaya ya Mbozi*) |
| CARITAS | Mradi wa Kilimo Mbeya |
| SUA | Sokoine University of Agriculture (*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo*) |
| TARP II | Tanzania Agricultural Research Project Phase Two ( *Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili*) |



Picha ya pamoja inayoonesha washiriki wa Warsha ya Kuimarisha Uhusiano Baina ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Iliyofanyika Katika Kituo cha Nazareti, Njombe13 - 15 Novemba 2000.

# Yaliyomo

**Dibaji** iii
**Vifupisho** v

1. UTANGULIZI ........ 1
   1.1 Ufunguzi wa warsha ........ 1
   1.2 Lengo na madhumuni ........ 1
   1.3 Washiriki wa warsha ........ 1
      1.3.1 Washiriki kutoka taasisi za utafiti ........ 1
      1.3.2 Washiriki kutoka mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ........ 1
      1.3.3 Washiriki wakulima ........ 2
   1.4 Matarajio ya washiriki ........ 2
   1.5 Uendeshaji wa warsha ........ 2
   1.6 Matokeo na kufunga warsha ........ 3

2. **MBINU YA UTATUZI YAKINIFU WA MATATIZO** ........ 3

3. **UHUSIANO WA MATATIZO NA UFUMBUZI WA MATATIZO YENYE KIPAUMBELE** ........ 3
   3.1 Matatizo makuu na dalili zake ........ 3
   3.2 Matatizo sababishi ya matatizo makuu na jinsi yanavyohusiana ........ 4
   3.3 Matatizo ya kupewa kipaumbele ........ 8
      3.3.1 Wakulima wa mahindi na viazi mviringo ........ 8
      3.3.2 Wakulima wa mpunga na ufugaji ........ 8
      3.3.3 Wakulima wa mahindi na ufugaji ........ 9

4. **MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA MATATIZO YENYE KIPAUMBELE** ........ 9

5. **HITIMISHO** ........ 14
   5.1 Ushiriki ........ 14
   5.2 Ufanisi wa mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo ........ 14
   5.3 Maandalizi na uendeshaji wa warsha ........ 14

| | | |
|---|---|---|
| Kiambatanisho Namba 1: | Maelezo kuhusu Mradi ........ | 15 |
| Kiambatanisho Namba 2: | Hotuba ya Ufunguzi ........ | 18 |
| Kiambatanisho Namba 3: | Orodha ya Washiriki wa Warsha ........ | 21 |
| Kiambatanisho Namba 4: | Maelezo ya kufunga Warsha ........ | 22 |
| Kiambatanisho Namba 5: | Hotuba ya Kufunga Warsha ........ | 24 |
| Kiambatanisho Namba 6a: | Kielelezo cha wakulima wa mahindi na viazi ...... | 26 |
| Kiambatanisho Namba 6b: | Kielelezo cha wakulima wa mpunga na ufugaji ... | 27 |
| Kiambatanisho Namba 6c: | Kielelezo cha wakulima wa mahindi na ufugaji ... | 28 |

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Ufunguzi wa Warsha

Kabla ya warsha kufunguliwa rasmi mwakilishi wa Mratibu wa Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya Profesa E. Batamuzi aliwaeleza washiriki (Kiambatanisho namba. 1) madhumuni ya Mradi na matarajio ya mradi kutoka katika warsha hiyo. Baadaye alimkaribisha mgeni rasmi Bw. T. Mssenga ambaye ni Kaîmu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Katika hotuba yake ya ufunguzi kwa washiriki (Kiambatanisho namba 2), Mgeni rasmi Bw. T. Mssenga aliwashukuru waandaaji wa warsha na kukipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa juhudi zake katika kuendeleza maisha ya mkulima mdogo kupitia Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya. Aliwasisitizia washiriki kuwa warsha hiyo ilikuwa ni moja ya mikakati ya kufanikisha malengo ya mradi huo.

## 1.2 Lengo na Madhumuni

Warsha iliandaliwa na Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo unaoendeshwa na Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo kikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway. Lengo la warsha lilikuwa ni kuamsha ari ya uhusiano baina ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima katika harakati za kuinua kipato na kuongeza uhakika wa chakula katika kaya. Madhumuni ya warsha yalikuwa yafuatayo:

1. Kujifunza mbinu shirikishi na endelevu katika kuainisha, kutambua matatizo na namna ya kuyapa kipaumbele.
2. Kuainisha matatizo yanayokabili kipato na chakula katika kaya.
3. Kuainisha matatizo yanayostahili kupewa kipaumbele katika utatuzi.
4. Kupendekeza ufumbuzi wa matatizo yaliyopewa kipaumbele.

## 1.3 Washiriki wa Warsha

Warsha ilishirikisha washiriki 36. Kati yao wakulima walikuwa 18, watafiti tisa, washauri watano, wataalamu watatu kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka kanda ya nyanda za juu kusini, na mwezeshaji mmoja. Katika jumla ya washiriki hao wanawake walikuwa 15 na wanaume 21. Washiriki wakulima wanawake walikuwa 8.

### *1.3.1 Washiriki kutoka taasisi za utafiti*

Taasisi za utafiti zilizokuwa na washiriki kwenye warsha ni:

1. Kituo cha utafiti wa kilimo Kifyulilo Songea
2. Kituo cha utafiti wa kilimo Uyole Mbeya
3. Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Morogoro

### *1.3.2 Washiriki kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs)*

Mashirika matatu yasiyo ya kiserikali yaliyokuwa na washiriki kwenye warsha ni:

1. CARITAS (Mradi wa kilimo Mbeya)
2. ADP (Kituo cha kuendeleza matumizi ya wanyamakazi wilaya ya Mbozi)

3. Small Holder Dairy Development Project (Mradi wa kuendeleza wafugaji wadogowadogo wa ng'ombe wa maziwa)

### *1.3.3 Washiriki wakulima*

Washiriki wakulima walitoka katika maeneo yenye aina tatu tofauti za kilimo ambazo ni:

1. Kilimo cha mpunga na ufugaji katika eneo la bonde la Usangu
2. Kilimo cha mahindi na viazi mviringo katika nyanda za juu kwenye milima ya Rungwe. Eneo hili pia hulimwa kahawa, chai na migomba.
3. Kilimo cha mahindi kwenye uwanda wa chini wa nyanda za juu katika Wilaya za Mbozi, na Iringa vijijini pia Mikoa ya Ruvuma na Rukwa. Eneo hili pia wapo wafugaji. Kilimo cha maharage pia ni maarufu.

## 1.4 Matarajio ya Washiriki

Washiriki walikuwa na matarajio mbalimbali kutokana na kushiriki kwao katika warsha hii. Wengi walitarajia kupata elimu na uzoefu wa namna ya kutatua matatizo yanayowakabili. Kwa ujumla matarajio ya washiriki yalikuwa:

1. Kupata elimu ya kilimo bora ili kuwaelimisha wakulima wengine.
2. Kufahamu vyema matatizo ya kilimo.
3. Kupata elimu ya kutatua matatizo ili kuinua kipato
4. Kuongeza hali ya kujiamini katika kufanya kazi za kilimo na ufugaji.
5. Kuongeza nguvu ya ufuatiliaji wa karibu kwa walengwa.
6. Kuona jinsi kaya inavyoweza kuhusishwa katika mradi huu.
7. Kuongeza maarifa juu ya kilimo cha mbegu.
8. Kujifunza mbinu bora za uzalishaji wa mazao na mifugo.
9. Kubadilishana uzoefu
10. Kuelewa namna ya kutatua matatizo.
11. Kupata elimu juu ya matumizi ya aina ya udongo na matumizi ya mbolea.
12. Kuelewa jinsi ya kushirikisha wakulima, washauri wa wakulima katika kuinua kipato cha wakulima mahali walipo.
13. Kuweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa chakula na kuongeza pato la mkulima.
14. Kupata msaada wa mbolea.
15. Kujua mipango ya mradi na utekelezaji wake.
16. Kuongeza ari ya kufanya kazi za ufugaji na kilimo.
17. Kupata ufumbuzi wa matatizo ya kilimo na ufugaji.
18. Kufahamu utafiti uliofanywa na wataalamu.
19. Kujifunza mbinu ya kuwahusisha washika dau.
20. Kujua namna ya kuboresha dhana ya ushirikishwaji.
21. Kuona kuwa matokeo ya utafiti yanakwenda sambamba na walengwa na yenye teknolojia sahihi kwa walengwa na washauri.
22. Mahusiano baina ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima yataongezeka.

## 1.5 Uendeshaji wa Warsha

Uendeshaji wa warsha uligawanyika katika sehemu kuu nne nazo ni:-

1. Kujifunza somo kuhusu mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo
2. Kujadili na kubaini matatizo na vyanzo vyake
3. Kutambua uzito baina ya matatizo ili kuyajua na kuyapa kipaumbele
4. Kujadili na kupendekeza ufumbuzi wa matatizo yaliyopewa kipaumbele.

Sehemu ya kwanza ilikuwa ni semina. Sehemu ya pili ilikuwa ni majadiliano ya washiriki wote kwa pamoja. Sehemu ya tatu na ya nne ilikuwa ni kazi za vikundi vilivyogawanyika kwa kutofautiana aina ya kilimo kama ilivyobainishwa kwenye aya namba 1.3.

### 1.6 Matokeo na kufunga warsha

Kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi kufunga warsha, mwakilishi wa Mratibu wa Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya Profesa E. Batamuzi alimfahamisha mgeni rasmi sehemu ya matokeo ya warsha hiyo (Kiambatanisho namba 4). Baadaye alimkaribisha mgeni rasmi Nd. A. Makiwa ambaye ni Afisa wa Kilimo na Mifugo wilaya ya Njombe kufunga warsha rasmi.

Katika hotuba yake ya kufunga warsha Kiambatanisho namba 5) kwa washiriki, mgeni rasmi Nd. A. Makiwa alionesha kuridhishwa kwake na matokeo ya warsha na kuwashukuru washiriki wote kwa juhudi waliyoonesha hadi kukamilisha malengo ya warsha hiyo. Mgeni rasmi alifunga warsha kwa kuwatakia kheri washiriki warudipo makwao.

## 2. MBINU YA UTATUZI YAKINIFU WA MATATIZO

Washiriki wote walipata fursa ya kujifunza juu ya mbinu yakinifu katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo. Mada ilitolewa kwa muda wa karibu nusu saa. Washiriki walijifunza namna ya kubaini matatizo kwa kuzingatia haja zilizopo. Pia walijifunza namna ya kubainisha uhusiano baina ya matatizo kwa jinsi yanavyosababishana. Baadaye walijifunza namna ya kutambua matatizo yanayostahili kupewa kipaumbele katika utatuzi. Waliuliza maswali mbalimbali na kudhihirisha kuwa walielewa somo hilo.

## 3. UHUSIANO WA MATATIZO NA UFUMBUZI WA MATATIZO YENYE KIPAUMBELE

Katika sehemu hii washiriki walianza kwa kutafakari haja za msingi zinazowafanya wajishughulishe na uzalishaji wa mazao na mifugo. Washiriki walibaini kuwa hali ya sasa ya haja hizo si ya kuridhisha. Hali hiyo ndiyo iliyowafanya washiriki wabaini matatizo makuu yanayokabili uzalishaji wa mazao na mifugo. Baadaye waliorodhesha matatizo yanayosababisha kuwepo kwa matatizo makuu na kuonesha jinsi matatizo hayo yanavyohusiana kwa jinsi ya kusababishana.

Baada ya kujua jinsi matatizo yanavyohusiana washiriki walifanya zoezi la kubainisha matatizo ya kupewa kipaumbele katika utatuzi. Kila eneo la aina ya kilimo kati ya maeneo matatu ya kilimo yaliyowakilishwa lilipata fursa ya kuonesha matatizo yanayostahili kupewa kipaumbele katika eneo lao. Baadaye washiriki kutoka katika maeneo hayo ya kilimo walitoa mapendekezo ya utatuzi wa matatizo ya mwanzo kupewa kipaumbele katika utatuzi kwenye eneo lao.

### 3.1 Matatizo makuu na dalili zake

Washiriki wa warsha walitafakari haja kuu zinazowafanya wajihusishe na **uzalishaji** wa mazao na mifugo. Ilibainika kuwa, haja kuu ni **lishe** na **kipato** cha kaya. Washiriki walibainisha kuwa hali ya lishe na kipato katika kaya bado ni **duni**. Kwa mujibu wa washiriki, vigezo vinavyobainisha kuwepo kwa hali duni ya kipato katika haya ni:-

1. Ukosefu wa fedha katika kaya.
2. Wazazi kushindwa kusomesha watoto wao.
3. Kushindwa kulipa kodi ya maendeleo.
4. Kushindwa kununua nyenzo bora.
5. Kuwa ombaomba.

6. Nyumba duni, za nyasi na miti zisizo safi wala imara.
7. Lishe duni.
8. Dhiki katika maisha ya kaya.
9. Kushindwa kumudu gharama za matibabu.
10. Mavazi duni.
11. Kuishi kwa kubahatisha bila kuwa na uhakika kuwa kaya itaishi vipi siku inayofuata.
12. Mavazi duni
13. Kilimo duni

Vigezo vinavyobaini kuwepo kwa lishe duni katika kaya ni:-

1. Afya duni hasa kwa watoto na kina mama.
2. Kaya kutokuwa na uhakika wa chakula, inahemea muda mwingi wa mwaka.
3. Uwezo mdogo wa kufanya kazi.
4. Utapiamlo na upungufu wa damu mwilini unaosababisha idadi kubwa ya vifo visivyo vya lazima.
5. Ukarimu kupungua.
6. Watoto kudumaa.

## 3.2 Matatizo sababishi ya matatizo makuu na jinsi yanavyohusiana

Washiriki, hususan wakulima, waliorodhesha matatizo yanayosabisha kuwepo kwa matatizo makuu. Orodha ya matatizo na maelezo yake imeoneshwa katika Jedwali namba 1.

Baadaye washiriki walijadili na hatimaye waliyapanga matatizo hayo kwa mtiririko unaoonesha matatizo hayo yanavyohusiana kwa jinsi ya kusababishana. Mtiririko huo ulikuwa katika hali ya mchoro ambao uliunganisha matatizo kwa mishale. Mshale ulikoelekea ulionesha tatizo **tokeo** na ulikoanzia ni tatizo **chanzo**. Kutokana na mtiririko huo washiriki walibaini kuwa tatizo kuu kuliko yote ni **lishe duni** na kwamba **kipato duni** pia kinasababisha kuwepo kwa **lishe duni**. Kutokana na mtiririko huo matatizo **chanzo** ya tatizo kuu yalibainishwa kuwa ni:

1. Ukataji miti hovyo
2. Serikali kuzuia umilikaji wa baadhi ya miti asili.
3. Ukataji miti holela.
4. Mila na desturi zilizopitwa na wakati.
5. Elimu duni ya lishe
6. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji.
7. Miundo mbinu hafifu.
8. Sera dhaifu ya Ushirika.
9. Masharti magumu ya kuuza mazao nje.
10. Wakulima kuzuiwa kuuza mazao nje ya nchi.
11. Pembejeo kuuzwa katika ujazo mkubwa kuliko mahitaji na uwezo wa mkulima/mfugaji.
12. Utaalamu ni gharama.
13. Washauri wa ugani wachache.
14. Ucheleweshaji wa majibu ya utafiti.
15. Ukosefu wa vitendea kazi kwa washauri wa ugani.
16. Wauzaji wa pembejeo hawana utaalamu.
17. Maslahi duni ya wafanyakazi.
18. Uthibiti mbovu wa ubora wa pembejeo.
19. Hali duni ya maisha vijijini.
20. Maamuzi katika kaya ya upande mmoja hasa baba.
21. Zana duni za kilimo na palizi.

22. Huduma duni ya maji kwa kilimo na mifugo.
23. Utafiti usiokamilika.
24. Magonjwa hasa UKIMWI.
25. Kutotambua kuwa mazao ya kilimo pia ni ya biashara.
26. Kupanda miti inayoharibu mazingira.
27. Uhaba wa ardhi.
28. Matumizi ya zana zisizo sahihi za usafirishaji.
29. Ukosefu wa zana sahihi katika baadhi ya maeneo.
30. Maghala na vihenge vibovu.
31. Wataalamu kutowajibika ipasavyo

Orodha kamili ya matatizo na maelezo yake imeoneshwa kwenye Jedwali namba 1.

## Jedwali namba 1. Orodha ya matatizo na maelezo yake

| | TATIZO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Lishe duni | • Kaya kutokuwa na chakula cha kutosha kwa siku nzima na kwa mwaka mzima<br>• Upungufu wa viini lishe muhimu katika milo ya kaya. |
| 2. | Kipato duni | • Kaya kutokuwa na kipato cha kutosha kukidhi mahitaji muhimu na ya lazima. |
| 3. | Mavuno duni | • Kaya kupata mavuno pungufu kuliko matarajio. |
| 4. | Chakula haba | • Kaya kuwa na chakula kidogo chini ya mahitaji. |
| 5. | Kutokuwa na soko la uhakika | • Kaya kutopata wanunuzi wa mazao na mifugo kwa wakati inapohitaji kuuza. |
| 6. | Bei ndogo ya mazao | • Kaya kuuza mazao kwa bei chini ya matarajio na isiyokidhi gharama za uzalishaji. |
| 7. | Wakulima kutokuwa na ushirikiano | • Wakulima kutokuwa na sauti ya pamoja kuhusu bei ya mazao yao na namna rahisi ya kupata pembejeo |
| 8. | Elimu duni ya lishe | • kaya kutotumia vyema viini lishe vilivyopo katika kaya. Mfano-Mayai, kuku, maziwa maharage karanga. Kaya inapodhani kuwa chakula ni mahindi, mpunga au mtama tu. |
| 9. | Serikali na kaya kutotambua kuwa mazao ya chakula pia ni ya biashara. | • Kaya inalima mazao ya chakula kwa lengo la kukidhi haja ya lishe ya kaya bila kulenga pia kuwa inahitaji ziada ya kuuza.<br>• Serikali kuwazuia wakulima wenye mavuno ya chakula wasiyauze bila kujali kuwa hayo ndiyo chanzo cha mapato kwa wakulima hao. |
| 10. | Serikali kutolinda soko la ndani | • Hali ya serikali kuagiza chakula nje au kuruhusu wafanyabiashara kuingiza chakula kutoka nje bila kuhakikisha kwanza chakula kilichopo nchini kimepata soko. |
| 11. | Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi ya uzalishaji | • Hali ya serikali kudhani kuwa kuna mvuno haba nchini kumbe yapo mavuno mengi au vinginenyo. |
| 12. | Masharti ya kuuza mazao nje ni magumu | • Wakulima kushindwa kuuza mazao yao nje ya nchi kutokana ukiritimba mwingi kupita kiasi uliopo serikalini kuhusu utoaji |

| | | |
|---|---|---|
| | | wa vibali vya kuuza mazao nje ya nchi. |
| 13. | Kutofuata kalenda ya kilimo | • Kulima na kupanda wakati usio, hasa kuchelewa.<br>• Kuhudumia mimea kwa wakati usiostahili mfano kupunguzia kahawa.<br>• Kuchelewa kupandisha au kuogesha wanyama. |
| 14. | Uharibifu wa mazingira | • Hali ya ardhi kuwa wazi bila mimea hasa miti. |
| 15. | Kukata miti ovyo | • Kukata miti bila utaratibu wa kuirudishia. |
| 16. | Uchomaji moto holela | • Kuungua kwa misitu na nyika bila kuwa na ulazima au bila mpangilio. |
| 17. | Maghala na vihenge vibovu. | • Maghala na vihenge visivyomudu kuzuia uharibufu wa mazao. |
| 18. | Kutotumia pembejeo | • Mazao au mifugo kuharibiwa au kudhuriwa na wadudu au magonjwa bila kutumia pembejeo zinazostahili. |
| 19. | Huduma hafifu ya maji kwa kilimo na mifugo | • Kiasi cha maji yanayopatikana shambani kwa ajili ya kumwagilia na kunywesha mifugo hakitoshi. |
| 20. | Hifadhi duni ya mazao na mifugo | • Ukosefu wa mbinu za uhakika za kuzuia uharibifu au wizi wa mazao na mifugo. |
| 21. | Magonjwa na wadudu waharibifu | • Mazao au mifugo kudhofika au kufa kutokana na maradhi<br>• Kuwepo wadudu waletao madhara katika mimea na mifugo |
| 22. | Uthibiti mbovu wa ubora wa pembejeo | • Wakulima kuuziwa pembejeo zilizokwisha pita muda wa kutumiwa au zisizofaa kabisa. |
| 23. | Mvua ya kutatanisha | • Mafuriko au ukame usiotarajiwa |
| 24. | Kulima shamba dogo | • Kaya kulima eneo dogo kuliko uwezo na mahitaji. |
| 25. | Kupanda miti inayoharibu mazingira | • Aina nyingine ya miti hunyonya maji na kukausha ardhi na vyanzo vya maji. |
| 26. | Uhaba wa ardhi | • Maeneo kutotosheleza mahitaji ya uzalishaji wa mazao na ufugaji |
| 27. | Wakulima hawawatumii wataalamu ipasavyo | • Kaya kutofuata ushauri ilioupata/kuona ili kuboresha kilimo |
| 28. | Mbinu bora za kilimo na ufugaji ni gharama | • Uwezo mdogo wa kugharamia mbinu bora za kilimo na ufugaji. |
| 29. | Pembejeo ghali | • Kaya kutomudu gharama za pembejeo zinazohitajika |
| 30. | Upatikanaji mgumu wa pembejeo | • Pembejeo hazipatikani kwa urahisi katika maeneo ya wakulima. |
| 31. | Upungufu wa nguvu kazi | • Kaya kutokuwa na uwezo wa kuhudumia mashamba au idadi ya mifugo inayohitajika kukidhi mahitaji muhimu ya Kaya |
| 32. | Magonjwa hasa UKIMWI | • Upungufu wa idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi kutokana na magonjwa na vifo |
| 33. | Matumizi yasiyo sahihi ya pembejeo | • Mkulima kutumia pembejeo kwa kipimo na aina tofauti ya jinsi inavyoshauriwa |
| 34. | Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa wakulima | • Pemebejeo zingine zinauzwa kwa ujazo ambao mkulima hauhitaji na hawezi kumudu gharama yake. |
| 35. | Wauzaji wa pembejeo hawana utaalamu | • Wauzaji wasio na utaalamu hutoa ushauri potofu kwa wakulima ili wapate biashara.<br>• Wauzaji kufumua bahasha au chupa za pembejeo ili kubadilisha |

| | | |
|---|---|---|
| | | vipimo vya ujazo na uzito bila kujali athari ya kufanya hivyo. |
| 36. | Matumizi mabaya ya mbolea. | • Kutumia kiasi kikubwa na mchanganyiko wa mbolea kinyume na ushauri |
| 37. | Upungufu wa rutuba | • Udongo kutokuwa na viini lishe vinavyohitajika katika mmea. |
| 38. | Mmomonyoko wa udongo | • Hali ya udongo wenye rutuba kuhamishwa. |
| 39. | Matumizi ya zana za usafirishaji zisizo sahihi. | • Zana zinazosababisha madhara katika udongo (mmomonyoko) au kupunguza thamani ya mazao yaliyobebwa kama kahawa mbichi na mchele ukiburuzwa kwenye chelezo cha mti kinacho vutwa na wanyamakazi. |
| 40. | Miundo mbinu hafifu | • Kaya kutokuwa na urahisi wa kusafiri au kusafirisha mazao/mifugo kufika sokoni |
| 41. | Gredi hafifu ya mazao | • Kaya kuwa na mazao yasiyo na ubora wa kupata soko au bei nzuri |
| 42. | Sera inayozuia umilikaji wa baadhi ya miti asili. | • Wakulima kutopanda au kuhifadhi na pengine kuhujumu baadhi ya miti ambayo ni muhimu katika kuhifadhi mazingira kwa sababu wao hawana nafasi ya kupata faida yoyote kutokana na kuhifadhi miti hiyo. |
| 43. | Uduni wa maisha vijijini | • Vijiji kutokuwa na urahisi wa kupata huduma za afya, elimu, maji |
| 44. | Vijana kukimbilia mijini | • Vijana kutopenda kujishughulisha na kilimo na ufugaji vijijini. |
| 45. | Zana duni za kilimo na palizi | • Matumizi ya nyenzo zisizo na tija |
| 46. | Mtaji mdogo | • Uwezo mdogo wa kumudu gharama za uzalishaji zinazohitajika |
| 47. | Ukosefu wa zana sahihi | • Matumizi ya zana zinazosababisha madhara katika uzalishaji |
| 48. | Mila na desturi zilizopitwa na wakati | • Mila zinazosababisha matumizi yasiyo ya lazima ya chakula na kipato<br>• Mila zinazozuia baadhi ya wana kaya hasa watoto na kina mama kula baadhi ya vyakula vyenye viini lishe muhimu. |
| 49. | Mipango mibaya ya matumizi ya chakula | • Kaya kutumia chakula au kipato bila mipangilio. Baba na mama kutojadiliana namna ya matumizi ya kaya |
| 50. | Maamuzi na umilikaji wa upande mmoja katika kaya hasa baba. | • Baba kufanya maamuzi ya pekee juu ya mali za kaya pamoja na chakula. (Baba anachukua lakini mama na watoto wanaiba). |
| 51. | Mahusiano hafifu katika kaya | • Wana kaya kufanya maamuzi ya kaya bila mawasiliano na makubaliano. |
| 52. | Elimu duni ya kilimo bora | • Kaya kutokuwa na mwamko juu ya mbinu bora za uzalishaji. |
| 53. | Majibu ya utafiti yanachelewa | • Matatizo yanayotokea kwa wakulima hayapati ufumbuzi wa kitaalamu haraka. |
| 54. | Utafiti usiokamilika | • Kupeleka utaalamu kwa wakulima bila kufanya tathmini ya ufanisi wa utaalamu huo katika eneo linlohusika. |
| 55. | Washauri wa ugani wachache | • Wakulima wengi hawana nafasi ya kuonana na washauri wa kilimo. |
| 56. | Wataalamu kutowajibika ipasavyo | • Wataalamu hawafanyi kazi inavyostahili |
| 57. | Ukosefu wa vitendea kazi | • Washauri kutofikia wakulima wengi kwa kutokuwa na zana za kazi na usafiri wa uhakika. |

## 3.3 Matatizo ya Kupewa Kipaumbele

Washiriki wakulima waligawanyika katika vikundi vitatu kufuata namna ya uzalishaji wa mazao na mifugo katika maeneo yao. Kila kikundi kilipata fursa ya kuonesha matatizo ya kupewa kipaumbele kwa kusambaza kete kwenye mchoro unaoonesha mtiririko wa uhusiano wa matatizo. Kila kikundi lilitengeneza nakala ya mchoro huo kwa kuzingatia matatizo yaliyo muhimu katika eneo lao.

Watafiti na washauri wa wakulima walisaidiana na wakulima katika kunakili michoro na kunakili idadi ya kete kadiri zilivyosambazwa kwenye michoro. Hatimaye, kila kikundi kilipata fursa ya kuwasilisha matokeo ya namna walivyoyapa kipaumbele cha utatuzi matatizo chanzo kwa konesha jinsi walivyogawanya kete kwenye mchoro wao.

Mgawanyiko wa kete katika michoro unaonekana katika vielelezo vilivyoambatanishwa kwenye Kiambatanisho 6a hadi 6c. Vielelezo hivyo vinaonesha kuwa kila kikundi kilitoa kipaumbele tofauti katika utatuzi wa matatizo *chanzo*. Miduara iliyozungushiwa mara mbili ni ile yenye matatizo *chanzo*. Nambari zilizomo ndani ya miviringo ni jumla ya kete zilizowekwa kwenye tatizo husika. Nambari zilizo kwenye mistari inaonesha idadi ya kete zilizohamishwa kutoka tatizo ***tokeo*** kwenda tatizo ***sababishi***. Matatizo chanzo ndiyo yanayotakiwa kutafutiwa ufumbuzi ili kutatua tatizo kuu.

### *3.3.1 Kikundi cha wakulima wa mahindi na viazi mviringo*

Kiambatanisho namba 6a kinaonesha mchoro wa kikundi hicho na namna kete zilivyosambazwa. Matatizo kumi ambayo kikundi hiki kiliyapa kipaumbele katika utatuzi ni:

1. Elimu duni ya lishe
2. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji.
3. Miundo mbinu hafifu
4. Sheria inyozuia umilikaji wa baadhi ya miti asili.
5. Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa wakulima.
6. Uthibiti mbovu wa ubora wa pembejeo.
7. Upandaji wa miti inayoharibu mazingira.
8. Sera dhaifu ya ushirika.
9. Maamuzi na umilikaji wa mali za kaya wa upande mmoja hasa baba.
10. Uchomaji moto holela.

Pamoja na kuwepo umuhimu wa kuimarisha elimu ya lishe katika kaya, mgawanyo wa kete katika mtiririko wa matatizo na jinsi yanavyosababishana (Kiambatanisho namba 6a) unaonesha kuwa kipaumbele katika utatuzi kilenge katika kuongeza uhakika wa soko ili kuinua kipato cha kaya. Aidha kipaumbele kilenge katika kuongeza matumizi bora ya pembejeo ili kuboresha mavuno na kuboresha hali ya mazingira ili hali ya mvua iweze kuwa ya uhakika na mavuno yaweze kuwa bora.

### *3.3.2 Wakulima wa mpunga na ufugaji*

Namna ambavyo kikundi hiki kiligawanya kete imeoneshwa kwenye mchoro, Kiambatanisho namba 6b. Matatizo kumi ya awali kupewa kipaumbele katika utatuzi, kwa mujibu wa kikundi hicho yalionekena kuwa ni:-

1. Huduma duni ya maji kwa mifugo na kilimo.
2. Miundo mbinu hafifu.
3. Wakulima kuzuiwa kuuza mazao nje.
4. Mila na desturi zilizopitwa na wakati.
5. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji.

6. Elimu duni ya lishe.
7. Mtaji mdogo.
8. Ukataji miti holela.
9. Masharti magumu ya soko la nje.
10. Sera ya ushirika ni dhaifu.

Mgawanyo wa kete katika mchoro wa mtiririko wa matatizo wa kikundi hicho (Kiambatanisho namba 6b) unasisitiza kuwa kuinua pato la kaya ni jambo muhimu zaidi katika kuboresha lishe ya kaya. Aidha kuinua pato la kaya na kuboresha lishe kunahitaji kuongeza wingi na ubora wa mavuno katika kaya. Kuwepo kwa soko la uhakika pia ni jambo muhimu katika kuinua pato la kaya. Pamoja na kuweka juhudi katika kuboresha huduma ya maji kwa kilimo na mifugo, ubora na wingi wa mavuno utahitaji matumizi bora ya pembejeo na kuwepo na kukabiliana na tatizo la mvua za kutatanisha.

### *3.3.3 Wakulima wa mahindi na ufugaji*

Mgawanyiko wa kete katika mchoro wa kikundi hicho (Kiambatanisho 6c) unaonesha kuwa matatizo kumi ya mwanzo kupewa kipaumbele ni:-

1. Elimu duni ya lishe.
2. Miundo mbinu hafifu
3. Uchomaji moto holela.
4. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji.
5. Kaya na serikali kutotambua kuwa mazao ya kilimo pia ni ya biashara.
6. Kupanda miti inayoharibu mazingira.
7. Matumizi mabaya ya mbolea.
8. Mitaji midogo.
9. Uthibiti mbovu wa ubora wa pembejeo.
10. Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa wakulima/wafugaji.

Pamoja na umuhimu wa kuboresha elimu ya lishe katika kaya ilionekana kuwa ufumbuzi unaolenga kutatua tatizo la mavuno duni ni muhimu zaidi katika kuondoa tatizo la lishe duni na kuinua pato la kaya. Kwa ujumla matatizo kumi ya mwanzo kupewa kipaumbele yanalenga katika kuwa na mipangilio bora ya matumizi ya chakula ili kuongeza wingi wa chakula katika kaya, kuboresha soko la mazao ili kuinua pato la kaya, na matumizi bora ya pembejeo na uboreshaji wa mazingira ili kuongeza wingi na ubora wa mavuno.

# 4. MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA MATATIZO YENYE KIPAUMBELE

Kila kikundi kilijadili na kutoa mapendekezo kuhusu ufumbuzi wa baadhi ya matatizo yaliyopewa kipaumbele. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwa washiriki wote na kujadiliwa kwa pamoja. Matatizo ambayo mapendekezo ya utatuzi wake yalijadiliwa ni:

1. Huduma duni ya maji kwa mifugo na kilimo.
2. Elimu duni ya lishe.
3. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji.
4. Miundo mbinu hafifu.
5. Sheria inyozuia umilikaji wa baadhi ya miti ya asili.
6. Pembejeo ghali.
7. Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa mkulima/mfugaji
8. Wakulima kuzuiwa kuuza mazao nje ya nchi.

Mapendekezo ya utatuzi wa matatizo hayo umeoneshwa kwenye Jedwali namba 2.

**Jedwali Na. 2. Mapendekezo ya ufumbuzi wa matatizo yenye kipaumbele**

| | TATIZO | UFUMBUZI | WATAFITI | WAKULIMA | WASHAURI | SERIKALI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Huduma duni ya maji kwa kilimo na mifugo | • Kuimarisha na kuboresha mifereji ya asili<br>• Kuboresha ugawaji wa maji<br>• Kuunda na kuimarisha vikundi vya watumiaji wa maji.<br>• Elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua<br>• Uchimbaji wa visima vya maji.<br>• Kuboresha utekelezaji wa sheria ndogondogo. | • Wafanye tathmini ya hali halisi ya mifereji<br>• Wabuni mbinu za kuboresha mifereji asili na matumizi ya maji.<br>• Watafute sababu ya vikundi kutofanya vizuri na kubuni mbinu ya kuviimarisha<br>• Wabuni mbinu rahisi na endelevu za uvunaji wa maji<br>• Watafiti maeneo mazuri yanayofaa kwa kuchimba visima<br>• Watafiti sababu zinazofanya sheria ndogondogo kutofuatwa | • Watoe taarifa halisi kuhusiana na hali halisi ya mifereji ilivyo<br>• Washiriki katika kuboresha na kutunza mifereji<br>• Wajiunge kwenye vikundi na kutengeneza utaratibu wa ugawanyaji wa maji.<br>• Washiriki mafunzo na kuzingatia utekelezaji<br>• Kushiriki katika uchimbaji visima na kuvitumia<br>• Wazingatie sheria ndogondogo za vikundi. | • Wawaandae wakulima washiriki kwenye tathmini ya mifereji na kubuni mbinu bora za matumizi ya maji<br>• Wawezeshe uundaji wa vikundi<br>• Washauri ushirikishwaji wa kina mama katika vikundi.<br>• Watoe tathmini ya maendeleo ya vikundi.<br>• Waelimishe wakulima juu ya matokeo ya utafiti.<br>• Watoe ushauri wa namna ya kutunza visima vya maji<br>• Wasaidie kufafanua sheria ndogondogo zilizowekwa | • Igharamie shughuli za ushauri na utafiti<br>• Igharamie uboreshaji na hifadhi ya vyanzo vya maji.<br>• Ivitambue vikundi kisheria na kuvipa ushirikiano katika kazi zake<br>• Kugharamia mafunzo<br>• Isaidie gharama za uchimbaji visima<br>• Isimamie utekelezaji wa sheria. |

| | TATIZO | UFUMBUZI | WATAFITI | WAKULIMA | WASHAURI | SERIKALI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Elimu duni ya lishe | • Tathmini ya ukubwa wa tatizo ifanywe<br>• Mafunzo ya vitendo na nadharia yafanywe kwa ngazi ya kaya (baba, mama na watoto). | • Wabuni mbinu rahisi na zinazokubalika katika kupata taarifa za hali ya lishe katika kaya.<br>• Watoe tathmini ya ukubwa wa tatizo kwa washika dau wote.<br>• Wabuni mchanganyiko wa viini lishe vinavyokubalika kulingana na mazingira<br>• Wabuni mbinu rahisi inayowezesha elimu ya lishe kuwafikia wanakaya wote.<br>• Wafanye utafiti utakaoshirikisha washika dau wote.<br>• Wafanye tathmini ya mafanikio. | • Watoe taarifa sahihi juu ya hali ya lishe katika kaya zao<br>• Washiri katika utafiti.<br>• Wazingatie na kutekeleza ushauri wa wataalamu<br>• Wafanye tathmini ya mafanikio. | • Watoe taarifa sahihi.<br>• Wawaandae wakulima kushiriki katika utafiti na kupokea ushauri.<br>• Watoe mafunzo na wafuatilie utekelezaji.<br>• Watoe taarifa ya mafanikio na matatizo kila inapolazimu | • Serikali za vijiji zishirikiane na wataalamu na kuweka mazingira mazuri ya mawasiliano.<br>• Serikali kuu igharimie utafiti na kutoa wataalamu.<br>• Wizara za afya, maendeleo ya jamii, kilimo na NGO washirikiane kikamilifu na wawe na mawasiliano baina yao. |

| | TATIZO | UFUMBUZI | WATAFITI | WAKULIMA | WASHAURI | SERIKALI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji | • Kumbukumbu na takwimu za uzalishaji ziboreshwe | • Wabuni mbinu rahisi na bora za ukusanyaji kumbukumbu kwa kuwashirikisha wakulima na washauri | • Watoe taarifa sahihi<br>• Watunze kumbukumbu za uzalishaji | • Wakusanye kumbukumbu zilizo sahihi katika hatua zote za uzalishaji<br>• Watoe mafunzo kwa wakulima juu ya kutunza kumbukumbu. | • Igharamie mafunzo na utafiti.<br>• Izitumie kumbukumbu hizo kuboresha soko la mazao ya wakulima.<br>• Serikali za vijiji ziwe na kumbukumbu ya maeneo ya uzalishaji. |
| 4 | Miundo mbinu hafifu | • Kuboresha miundo mbinu vijijini | • Watafiti juu ya miundo mbinu muafaka na bora | • Wahusike katika kuboresha na kusimamia miundo mbinu | • Watoe ushauri juu ya uboreshaji wa miundo mbinu | • Ihamasishe wakulima kushiriki katika uimarishaji wa miundo mbinu<br>• Serikali kuu na za mitaa zigharamie katika uboreshaji miundo mbinu. |
| 5 | Sheria inayozuia umilikaji wa baadhi ya miti asili | • Sheria za namna hiyo zibadilishwe | • Wafanye utafiti juu ya athari ya sheria hizo na waishauri Serikali ipasavyo | | | • Ibadilishe sheria hiyo |

| | TATIZO | UFUMBUZI | WATAFITI | WAKULIMA | WASHAURI | SERIKALI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa wakulima | • Pembejeo ziuzwe katika ujazo na uzito ambao mkulima mdogo anahitaji na anaweza kumudu. | • Wafanye utafiti juu ya ujazo muafaka | • Watoe ushauri kwa mawakala wa pembejeo juu ya ujazo muafaka wa pembejeo. | • Watoe ushauri kwa mawakala wa pembejeo juu ya ujazo muafaka wa pembejeo. | • Itoe maagizo juu ya mapendekezo ya ujazo muafaka kwa taasisi na makampuni husika kulingana na ushauri wa wataalamu. |
| 7 | Pembejeo ghali | • Matumizi ya madawa, mbolea na mbinu asili za uzalishaji ziimarishwe | • Watafiti mbinu bora za asili zina zofaa kutumiwa | • Wakulima wawe tayari kutumia mbinu asili katika uzalishaji. | • Watoe mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu za asili za uzalishaji. | • Serikali igharamie utafiti na ushauri juu ya matumizi ya mbinu asilia<br>• Iboreshe sera ya ushirika ili pembejeo ziweze kuwafikia wakulima kwa urahisi. |
| 8 | Wakulima kuzuiwa kuuza mazao nje ya nchi | • Kuimarisha ushirika na uimarishaji wa vikundi vya wakulima/wafugaji<br>• Ushirikiano na mitandao ya wakulima na wafanyabiashara wa ndani na nje | • Wafanye utafiti wa hali ya masoko ya mazao ya ndani na nje. | • Washiriki katika maonyesho mbalimbali ya kibiashara<br>• Wadumishe ubora wa mazao | • Wawaelimishe wakulima kuhusu ushirika<br>• Wasimamie uundaji wa vikundi vya ushirika<br>• Wasimamie uzalishaji wa mazao na mifugo bora | • Serikali ilegeze masharti ya soko la nje<br>• Serikali igharamie vikundi vya wakulima kushiriki katika mafunzo na maonyesho ya kibiashara |

# 5. HITIMISHO

Hali ya ushiriki wa washiriki katika vipindi vyote na ufanisi wa mbinu iliyotumika ilionesha kuwa ni ya kuridhisha. Kwa ujumla warsha ilimalizika kwa mafanikio ya kuridhisha kulinganisha na madhumuni yake na matarajio ya washiriki kwa mujibu wa tathmini ya washiriki wenyewe.

## 5.1 Ushiriki

Washiriki waliweza kuelewa somo juu ya mbinu iliyotumiwa, na waliweza kuitumia bila usumbufu. Kazi za vikundi zilifanywa kwa bidii na ushirikiano wa hali ya juu. Mchanganyiko wa kijinsia na wa wataalamu na wakulima uliboresha zaidi mafanikio ya warsha. Washa hii imekuwa kielelezo hai juu ya namna ambavyo kina mama na kina baba wanavyoweza kufanya kazi kwa pamoja bila kujali jinsia. Aidha, imedhihirisha jinsi wakulima wanavyoweza kushirikiana kikamilifu na wataalamu katika kupanga na kuweka mikakati ya maendeleo.

Hakukuwa na jambo lolote la dhahiri lililoonesha udhaifu katika ushiriki. Hata hivyo katika tathmini washiriki wawili hawakupendezwa na jinsi ambavyo baadhi ya washiriki walivyotumia lugha mchanganyiko, kiswahili na kiingereza, katika kuchangia hoja.

## 5.2 Ufanisi wa mbinu ya utatuzi yakinifu wa matatizo

Kwa mara nyingine mbinu hii ambayo ilibuniwa hasa kutumika kwenye mazingira ya nje (field) imeonesha ufanisi mkubwa wa kutumiwa kwenye mazingira ya ndani. Washiriki waliweza kuitumia mbinu hiyo bila matatizo ingawa wengi wao waliona kuwa muda ulikuwa mfupi mno ili kuifahamu mbinu hiyo kikamilifu.

## 5.3 Maandalizi na uendeshaji wa warsha

Washiriki wengi waliridhishwa na maandalizi na jinsi warsha ilivyoendeshwa. Asilimia 55 ya washiriki 31 waliofanya tathmini ya mwenendo wa warsha waliona kuwa warsha ilikidhi matarajio yao kwa kiwango kikubwa. Asilimia 31 waliona kuwa matarajio yao yalifikiwa kiasi, yaani chini ya asilimia 50 ya matarajio na asilimia 14 ya washiriki waliona kuwa matarajio yao yamefikiwa kwa wastani, yaani asilimia 50.

Tatizo kubwa lililowakera washiriki wengi ni muda wa warsha kuwa mfupi kiasi cha kulazimu kufanya kazi nje ya muda wa kazi. Asilimia 54 kati ya washiriki 32 waliofanya tathmini walikerwa na tatizo hilo. Wengi wao walipendekeza kuwa muda wa warsha uwe siku 4 au 5. Wengine walipendekeza muda wa kufungua na kufunga warsha ufupishwe ili muda wa kazi uongezeke. Washiriki wengine walipendekeza kuwa idadi ya milo ipungue ili kufidia muda wa ziada unaotakiwa na pia gharama inayopungua waongezewe washiriki katika fedha yao ya mfukoni (pocket money). Mshiriki mmoja alishauri kuwepo na ziara ya kutembelea wakulima kwenye ratiba ya warsha ili washiriki waweze kuthibitisha baadhi ya matokeo ya warsha kwa kuzungumza na wakulima wenyeji.

# KIAMBATANISHO NAMBA 1:

## Maelezo Kuhusu Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania

**Mradi wa Utafiti Unaotilia Mkazo Wanawake**

Yalitolewa na Profesa E. Batamuzi kwa Niaba ya Mratibu wa Mradi (Profesa L. D. B. Kinabo) Kwenye Warsha ya Uimarishaji wa Uhusiano Kati ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, katika Kituo cha Nazareti, Njombe.
tarehe 13 - 15 Novemba 2000

## Shukrani

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe,
Mkuu wa kituo cha Nazareti,
Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
Mabibi na Mabwana.

Kwa niaba ya Timu ya Utekelezaji wa **Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania,** na kwa niaba yangu binafsi, napenda kuchukua fursa hii kusema karibuni sana kwenye hii warsha inayofanyika chini ya mradi huu. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa washiriki wote waliopo hapa kwa kuitikia mwito wetu wa kushiriki kwenye hii warsha.

*Mkurugenzi Mtendaji. Tumeonelea ni vyema kabla ya kukukaribisha rasmi kutufungulia hii warsha,* tutoe maelezo machache kuhusu mradi huu.

## Utangulizi

Kwa kutambua kuwa kilimo ndiyo sekta mama ya uchumi na mhimili mkubwa wa chakula katika nchi hii, na hisia kwamba kilimo hakijaendelezwa kikamilifu, Serikali ya Tanzania imeamua kutilia mkazo kwenye utafiti wa kilimo kama mojawapo ya nyezo muhimu za kuendeleza kilimo. Hivyo basi lengo kubwa la utafiti wa kilimo kama ilivyotamkwa kwenye sera ya kilimo ya mwaka 1997, ni kuboresha uhakika wa chakula na pato la kaya, kuongeza ajira na masoko ya nje kwa kubuni, kutumia na kukuza mbinu zinazofaa na ambazo hazina madhara kwenye mazingira.

Katika kutekeleza sera hii, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilianzisha mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili (Tanzania Agricultural Research Project Phase Two - TARP II). Wahisani mbali mbali, waliokubali kugharamia mradi huu ni kama vile Benki ya dunia, Serikali za nchi za Uholanzi, Denmark, Uingereza na Norway. Wahisani hawa wanasaidia kanda tofauti tofauti nchini. Serikali ya Norway kwa kupitia Shirika lake la Maendeleo *yaani NORAD, limekubali kusaidia utafiti* katika Kanda mbili. Hizi ni: Kanda ya Mashariki inayojumuisha Tanga, Dar es Salaam, Pwani na

Morogoro, na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Iringa. Mradi ambao unatekelezwa chini ya msaada wa NORAD, ni huu nilioutaja hapo awali yaani Uhakika wa Chakula na Pato la kaya kwa wakulima wadogo wadogo. Shirika la NORAD limeidhinisha kiasi cha Shillingi za Kitanzania billioni tano kwa kipindi cha miaka minne kuanzia Septemba 2000. Mradi huu unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway. Hivyo basi, Mradi huu ni kati ya tafiti mbalimbali zinazofanywa chini ya mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili (TARP II).

## Lengo

Mabibi na Mabwana. Lengo kuu la mradi ni kuimarisha uhakika wa chakula na pato la kaya kwa wakulima wadodo wadogo na hasa wanawake.

## Kusudi

Mradi unakusudia kubuni na kusambaza kwa matumizi ya wakulima wadogowadogo teknolojia zinazoweza kuboresha uhakika wa chakula na pato la kaya.

## Matokeo

Matokeo yanayotarajiwa yako makuu matano:

1. Kwanza, ni matokeo ya tafiti za kilimo zinazolenga matatizo ya wakulima wadogowadogo. Rasimu ya tafiti hizi zinaandaliwa na watafiti wa Chuo wakishirikiana na wale wa Wizara ya Kilimo pamoja na wale wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway.
2. Pili, ni kuimarishwa kwa uhusiano kati ya watafiti, wakulima na washauri wa kilimo vijijini. Warsha ya leo ni mojawapo ya njia mbali mbali ambazo zinatumika kuimarisha uhusiano huo.
3. Tatu, ni wahitimu 32 wa Wizara ya Kilimo wenye shahada za juu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Wanafunzi hawa wameshadahiliwa na Chuo na wako masomoni tayari.
4. Nne, ni rasimu ya mapendekezo kwa Serikali na wahisani juu ya mfumo endelevu wa kugharamia shughuli za utafiti wa kilimo. Maandalizi ya kutayarisha rasimu hiyo yamekwisha anza, na mzabuni atakayepewa kazi hii anatarajiwa kutangazwa mwezi Desemba.
5. Tano, ni tathmini ya mabadiliko yatokanayo na tafiti zilizokwishafanyika na zinazofanyika sasa. Maandalizi pia ya kazi hii yamekwisha anza.

## Walengwa

Walengwa wakuu wa mradi huu ni wakulima waliopo kwenye kanda zifuatazo:

1. Kanda ya Mashariki inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.
2. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, inayojumuisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, na Rukwa.

## Ushirikishwaji wa wakulima

Kuhusu ushirikishwaji, Mradi unasisitiza ushirikishwaji wa wakulima katika hatua zote muhimu za kufanya utafiti, unaolenga masilahi yao.

## Faida kwa Wakulima kushiriki

Swali ambalo linaweza kuulizwa, ni kama kuna faida yeyote kwa wakulima kushiriki katika kutekeleza huu mradi. Tunasema ni vyema wakulima kushiriki kwa sababu wao ndiyo walengwa. Faida watakazozipata ni pamoja na:

1. Kupata elimu na mbinu bora za kutatua matatizo yanayowakabili kwenye kilimo
2. Ongezeko katika uzalishaji mazao
3. Ongezeko la kipato

## Motisha

Kuhusu motisha, ni kwamba, wakulima, watafiti na washauri watakaoonekana wamefanya bora zaidi watatunukiwa vyeti maalum na fedha taslimu kwa lengo la kuongeza ari. Fedha zitakazotolewa kwa wakulima kila mwaka na kila kanda ni kama zifuatazo:

1. Mkulima atakayeshinda nafasi ya kwanza, atatunukiwa shillingi 200,000
2. Mkulima atakayeshinda nafasi ya pili, atatunukiwa shillingi 100,000
3. Mkulima atakayeshinda nafasi ya tatu, atatunukiwa shillingi 75,000
4. Aidha wakulima wote hawa watatu watatunukiwa vyeti maalum.

## Mwisho

Ni matumaini yangu kuwa, kwa haya mafupi, washiriki wa warsha hii wamepata muhtasari wa mradi huu wa Uhakika wa chakula na pato la kaya ulivyo; na sina shaka kuwa wataendelea kushirikiana nasi ili lengo la mradi liweze kufanikiwa.

Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kumkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe aifungue rasmi Warsha hii.

Mkurugenzi Mtendaji.

# KIAMBATANISHO NAMBA 2:

**Hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Kwenye Ufunguzi wa Warsha ya Uimarishaji wa Uhusiano baina ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**

Iliyofanyika tarehe 13-15 Novemba 2000, katika Kituo cha Nazareti, Njombe.

---

Mwakilishi wa Mratibu wa Mradi,
Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
Mwenyekiti wa Warsha,
Mabibi na Mabwana

1. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandaji wa warsha hii muhimu kwa kunialika kujumuika nanyi wote kwenye sehemu ya ufunguzi.

2. Pili, kwa wale washiriki wote wanaotoka nje ya Wilaya ya Njombe, napenda niwakaribishe kwa moyo wa dhati kabisa Wilayani hapa, na ninawaombeni mujisikie nyumbani kwa muda wote mtakaokaa hapa. Karibuni sana; hii ni Wilaya yenu.

3. Mabibi na Mabwana. Warsha hii ni ya kipekee kwa kuwa imewajumuisha pamoja wakulima, watafiti na washauri wa kilimo kutafakari kuhusu maeneo ambayo yatafanyiwa utafiti ili kuweza kuchangia katika kutatua matatizo yanayowakabili wakulima wadogo wadogo wa nchi hii. Lengo kubwa ni kuinua maisha ya wakulima kwa kuboresha uhakika wa chakula na kuongeza pato la kaya kwa wakulima wadogowadogo hasa wanawake.

4. Kuandaa warsha za namna hii ni moja ya majukumu ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine katika kuwa karibu zaidi na wakulima na watendaji wa mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali ili kuchangia kwa karibu katika kuleta maendeleo ya kilimo kwa ujumla.

5. Nimeelezwa kuwa warsha hii ni moja kati ya mikakati mbali mbali inayotumika katika kutekeleza mradi huu wa UHAKIKA WA CHAKULA NA PATO LA KAYA KWA WAKULIMA WADOGO WADOGO TANZANIA. Hivyo basi, uimarishaji wa uhusiano kati ya wakulima, watafiti na washauri wa kilimo kwa lengo la kuongeza uhakika wa chakula na pato la kaya ni kati ya mikakati hiyo ya mradi.

6. Mabibi na mabwana, inaaminika kwamba kuunganisha nguvu na mawazo ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima huzaa matunda na kuhakikisha maendeleo endelevu. UTAFITI huleta elimu mpya, mbinu mpya na teknolojia mpya katika kuyamudu maisha ya binadamu. Hizi ni zana muhimu za kuboresha kilimo. Aidha ni zana ambazo zinachangia kwa kiwango kikubwa katika kuboresha matumizi ya muda na hivyo kupunguza muda mwingi ambao wakulima hasa kina mama hutumia katika kazi za shambani.

USHAURI WA KILIMO husaidia kuelimisha na kusambaza teknolojia hiyo kwa wakulima na pia kuwapatia ushauri wa umuhimu na matumizi ya teknolojia. WAKULIMA nao kwa upande wao hushauriwa kupokea teknolojia hiyo, kuijaribu katika mashamba yao, kutoa maoni yao kuhusu teknolojia na ushauri waliopewa. Aidha wakulima wana jukumu la kushauri, kupendekeza, pamoja na kuhamasisha wakulima wengine washiriki katika matumizi ya teknolojia ambayo imeonekana kuwa ya manufaa. Kwa kutambua yote haya, mradi unasisitiza kuwa watafiti hawana budi kuwashirikisha wakulima katika hatua zote muhimu za kufanya utafiti, ambazo ni:

- Kuchambua matatizo,
- Kupanga mipango,
- Kutekeleza na
- Kusambaza matokeo kwa ajili ya matumizi.

7. Nimeelezwa kuwa madhumuni ya warsha hii ni kama yafuatayo:

Kwanza, ni kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo.

Pili, ni kuchambua na kuanisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogo wadogo.

Tatu, ni kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi.

Nne, ni kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

8. Mabibi na Mabwana. Nimeelezwa vilevile kuwa washiriki wametoka katika kanda ya nyanda za juu kusini ambao ni wakulima 18 kutoka katika maeneo (farming systems) matatu tofauti, watafiti sita kutoka katika vituo vya utafiti vilivyopo katika kanda hii, washauri watano wa kilimo kutoka vijijini, na wawakilishi watatu wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

9. Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi, katika kutekeleza mradi huu Chuo kinashirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH). Ipo miradi mingine mingi ya utafiti inayofanywa na Chuo kwa kushirikiana na Vyuo vingine na taasisi mbali mbali duniani.

10. Hivyo basi, Chuo kina dhamana kubwa katika kuhakikisha kuwa mradi huu unafanikiwa kwa kushirikiana na vyombo vingine muhimu. Ni imani yangu kwamba kuhusika kikamilifu kwa idara mbali mbali za wizara na mashirika mengine katika kuandaa warsha hii ni mchango mmoja wapo katika kutekeleza malengo ya mradi huo. Sina shaka kwamba moyo huu wa ushirikiano utaendelea.

11. Mabibi na Mabwana. Mradi huu unatoa changamoto kubwa na nafasi kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na washirika wake kubuni na kufanya tafiti ambazo ni za kutatua matatizo ya kilimo cha nchi hii. Hivyo nachukua nafasi hii kuwashauri watafiti wa SUA na pengine hata Wizara ya Kilimo na Ushirika kuhakikisha mradi huu unafanikiwa kwa kufanya tafiti ambazo zitaleta matunda haraka iwezekanavyo. Ni nani ambaye hajui kuwa mwenye njaa hawezi kuambiwa ngoja kesho?

12. Baada ya kusema hayo machache napenda kutoa shukrani za dhati kwa Shirika la Maendeleo la Norway yaani NORAD ambalo ndilo mhisani mkuu wa mradi huu. Kama siyo kwa msaada wao mkubwa, mradi huu usingelifikia hapa ulipo. Aidha napenda kuwapongeza na kuwashukuru waandaji wa warsha hii, na kwa kunikaribisha kuja kuifungua. Ni imani yangu kuwa washiriki wote mtaitumia fursa hii kutoa mapendekezo muafaka ya maeneo ya kufanyia utafiti, na kwamba mtafurahia kukaa kwenu hapa Njombe. Jisikieni huru kutembelea sehemu mbali mbali za mji huu mara mpatapo nafasi ya kufanya hivyo. Nawatakieni kila la kheri na ufanisi kwenye warsha hii.

13. Mabibi na mabwana. Mwisho, napenda niseme nafurahi kutamka kuwa warsha ya UIMARISHAJI WA UHUSIANO KATI YA WATAFITI, WAKULIMA NA WASHAURI WA WAKULIMA WA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI imefunguliwa rasmi.

*ASANTENI SANA.*

## KIAMBATANISHO NAMBA 3:

## Orodha ya Washiriki wa Warsha

| | Jina | Kundi | Anwani |
|---|---|---|---|
| 1. | Edith Mwaikambo | Mshauri | SLP 98 Chimala Mbeya |
| 2. | Zakia Halfani Matumula | Mshauri | SLP 253 Mbeya |
| 3. | Renato C. Makafu | Mshauri | SLP 664 Makambakao |
| 4. | Nuhu Y. Mohamedi | Mshauri | SLP 168 Njombe |
| 5. | Adelaide E. Ngali | Mshauri | SLP 995 Songea |
| 6. | Anthony Kisengo | CARITAS | SLP 179 Mbeya |
| 7. | Abel M. Mbwile | ADP | SLP 204 Mbeya |
| 8. | Yahya A. K. Mshana | SURUDE | SLP 252 Iringa |
| 9. | Amasidze Mwangike (Bi) | Mkulima | SLP 34 Ilembula Mkakambako |
| 10. | Hamza Katimba | Mkulima | SLP 89 Rujewa Mbeya |
| 11. | Rehema Mfumbilwa (Bi) | Mkulima | SLP 73 Ilembula |
| 12. | Sweetheart Chiapo | Mkulima | SLP 766 Songea |
| 13. | Tabia .W. Mwansembo (Bi) | Mkulima | SLP 204 Mbozi Mbeya |
| 14. | Philemon Katela Mbegani | Mkulima | SLP 865 Mbeya |
| 15. | Mwawa Mkwamu | Mkulima | SLP 4508 Mbeya |
| 16. | Joyce Kihahwe (Bi) | Mkulima | SLP 11 Njombe |
| 17. | Huruma Mhapa | Mkulima | SLP 323 Njombe |
| 18. | Conrada C. Milinga (Bi) | Mkulima | SLP 7 Peramiho Songea |
| 19. | Atu Nkosya (Bi) | Mkulima | SLP 29 Chimala Mbeya |
| 20. | Damiani Nyudike | Mkulima | SLP 11 Njombe |
| 21. | Joseph E. Luvanja | Mkulima | SLP 46 Njombe |
| 22. | Chilanga Nyato (Bi) | Mkulima | SLP 973 Makambako |
| 23. | Rehema M. Nyato (Bi) | Mkulima | SLP 1115 Makambako |
| 24. | Jumanne S. Nkanyanga | Mkulima | SLP 313 Mbeya |
| 25. | Edward M. Mogha | Mkulima | SLP 139 Mbeya |
| 26. | Tobias Mwaliva | Mkulima | SLP 185 Mafinga |
| 27. | Esther E. Meela | Mtafiti | SLP 400 Mbeya |
| 28. | Josephath A. Kamasho | Mtafiti | SLP 400 Mbeya |
| 29. | R. P. Mbwile | Mtafiti | SLP 400 Mbeya |
| 30. | Rose Mongi-Henday | Mtafiti | SLP 400 Mbeya |
| 31. | Michael S.C. Mhosole | Mtafiti | SLP 93 Mufindi |
| 32. | Ahaz N. Mussei | Mtafiti | SLP 400 Mbeya |

**'Waandaji**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33. | Joyce Lyimo-Macha | Mtafiti | SLP 3000 SUA |
| 34. | E. Batamuzi | Mtafiti | SLP 3000 SUA |
| 35. | P. Makungu | Mtafiti | SLP 3000 SUA |
| 36. | A. M. Bakari | Mwezeshaji | SLP 3000 SUA |

## KIAMBATANISHO NAMBA 4:

**Ufungaji wa Warsha ya Uimarishaji wa Uhusiano Baina ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima, 13 - 15 Novemba, 2000**

Mgeni Rasmi,
Mwakilishi wa Mkurugenzi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
Mwenyekiti wa Warsha,
Mabibi na Mabwana.

1. Napenda kuchukua fursa hii kutoa muhtasari kuhusu Warsha hii kabla ya kumkaribisha rasmi, Mgeni wetu atufungie Warsha hii.

2. Mgeni Rasmi. Warsha hii ambayo ilianza juzi, ni moja ya shughuli muhimu za kutekeleza mradi wa "Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania".
Lengo la Warsha lilikuwa ni kuimarisha uhusiano kati ya watafiti, wakulima vijijini na washauri wa wakulima. Warsha ilishirikisha washiriki 36. Kati yao wakulima walikuwa 18, watafiti tisa, washauri watano, wataalamu watatu kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na mwezeshaji mmoja. Katika jumla ya washiriki hao wanawake walikuwa 15 na wanaume 21. Washiriki wakulima wanawake walikuwa 9.

3. Washiriki waliorodhesha matarajio yao baada ya warsha. Aidha walibaini haja kuu zinazofanya kaya zijishughulishe na kilimo, na kubaini hali ilivyo kuhusiana na haja hizo.

4. Waliorodhesha dalili za kipato kidogo, na dalili za lishe duni.

5. Washiriki wamepata fursa ya kujifunza jinsi ya kuchambua vyanzo na masababisho ya matatizo yaani "mbinu ya utatuzi yakinifu". Wakulima walitumia mbinu hii na uzoefu wao kubainisha matatizo yanayowakabili kwenye shughuli zao za kilimo.

6. Tatizo la msingi lililobainishwa ni mavuno duni. Aidha, walibainisha kuwa, hili tatizo linaleteleza lishe duni, na kipato kidogo cha kaya, mambo ambayo ni kioo cha umaskini. Baadhi ya sababu ambazo Wakulima wamezibainisha kuwa zinachangia kwenye mavuno duni ni:

    1. Huduma duni ya maji kwa kilimo na mifugo
    2. Elimu duni ya lishe
    3. Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za uzalishaji
    4. Miundo mbinu hafifu
    5. Sheria inayozuia umilikaji wa baadhi ya miti asili
    6. Ujazo mkubwa wa pembejeo kuliko mahitaji na uwezo wa wakulima
    7. Pembejeo ghali
    8. Wakulima kuzuiwa kuuza mazao yao nje ya nchi

7. Haya yalipambanuliwa na kupewa kipaumbele katika kupendekeza utatuzi. Mapendekezo kadhaa ya kutatua matatizo hayo yamejadiliwa.

8. Mgeni rasmi, yote haya yamefanywa na washiriki wote kwa pamoja na kwa ushirikiano mkubwa. Ni imani yetu kuwa moyo huu utaendelea kwa siku zijazo, kwani warsha za aina hii zimepangwa

kufanyika mara mbili kila mwaka, kwa kila kanda. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa, kwa washiriki na waandaaji wote waliowezesha warsha hii kufanikiwa.

9. Mabibi na Mabwana, kwa maneno haya machache, napenda kuchukua nafasi hii kumkaribisha rasmi, mgeni wetu Bwana Makiwa, Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya ya Njombe atufungie Warsha yetu.

Mgeni Rasmi.

**KIAMBATANISHO NAMBA 5:**

## Hotuba ya Bwana A. Makiwa, Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya ya Njombe, Kwenye Ufungaji wa Warsha ya Uimarishaji wa Uhusiano Kati ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Iliyofanyika Tarehe 13-15 Novemba 2000, Kituo cha Nazareti, Njombe, Iringa.

Mratibu wa mradi
Mkurugenzi wa kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
Mwenyekiti wa warsha,
Mabibi na Mabwana

1. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandaaji wa warsha hii muhimu kwa kunialika kujumuika nanyi wote kwenye sehemu ya ufungaji.

2. Pili, kwa wale washiriki wote wanaotoka nje ya wilaya ya Njombe, napenda niwakaribishe tena wilayani hapa, na nina imani kuwa mmefurahia kukaa kwenu Njombe.

3. Mabibi na Mabwana. Nimeelezwa kuwa hii ni warsha ya kipekee kwa kuwa imewajumuisha pamoja wakulima, watafiti na washauri wa kilimo kutafakari kuhusu maeneo ambayo yatafanyiwa utafiti ili kuweza kutatua matatizo yanayowakabili wakulima wadogo wadogo wa nchi hii. Lengo kubwa ni kuinua maisha ya wakulima kwa kuboresha uhakika wa chakula na kuongeza pato la kaya kwa wakulima wadogowadogo hasa wanawake.

4. Ili kuwa karibu zaidi na wakulima na watendaji wa mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali, warsha za namna hii ni moja ya majukumu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika kuleta maendeleo ya kilimo kwa ujumla.

5. Nimeelezwa kuwa warsha hii ni moja kati ya mikakati mbali mbali inayotumika katika kutekeleza mradi huu wa UHAKIKA WA CHAKULA NA PATO LA KAYA KWA WAKULIMA WADOGO WADOGO TANZANIA. Hivyo basi uimarishaji wa uhusiano kati ya wakulima, watafiti na washauri wa wakulima kwa lengo la kuongeza uhakika wa chakula na pato la kaya ni kati ya mikakati hiyo ya mradi.

6. Mabibi na Mabwana, nimeelezwa kuwa warsha hii imewajumuisha wakulima 18 wa mazao na mifugo mbali mbali, watafiti tisa, washauri wa wakulima 5 na wawakilishi 3 wa mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuendeleza kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima na kupanga mikakati ya kutatua matatizo hayo.

7. Nimeelezwa kuwa madhumuni ya warsha hii ni
   a).Kuchambua na kuanisha matatizo yanayowakabili wakulima.
   b). Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe kipaumbele zaidi.
   c). Kushiriki katika kuorodhesha mikakati au mbinu za kupata utatuzi wa matatizo hayo.

8. Nimeelezwa vilevile kuwa kwa kushirikiana, washiriki wamepata nafasi ya kujadili na kuchambua matatizo mbali mbali yanayowakabili wakulima kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

9. Mabibi na Mabwana, orodha mliyotayarisha ya mikakati iwe ndio muongozo wa namna mtakavyotatua matatizo mliyoyaainisha. Hili sio kwa wakulima tu. Ninayo imani kuwa watafiti mashirika yasiyo ya kiserikali na washauri wa wakulima nao watakuwa na majukumu yao ambayo yatahitaji utekelezaji wa haraka na endelevu.

10. Nimedokezewa kuwa kabla ya kuanza warsha hii mlitayarisha orodha ya matarajio yenu baada ya kutoka hapa. Nafurahi kusikia kuwa malengo na matarajio mengi ya washirika yametimizwa.


11. Baada ya hayo napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa kushiriki katika warsha hii, na kwa kunikaribisha kuja kuifunga. Naamini mtautumia ujuzi mlioupata katika kupanga mikakati endelevu ya kutatua matatizo mliyoyachambua na pia kupanga mapendekezo muafaka ya maeneo ya kufanyia utafiti. Jambo muhimu zaidi ni kuwaomba mzidi kuimarisha uhusiano kati yenu ili kutimiza malengo yenu ya kuwa na uhakika wa chakula na ongezeko la pato katika kaya za wakulima wadogo wadogo. Nawatakieni kila la kheri mrudipo makwenu.

12. Mabibi na Mabwana, napenda kutoa shukrani nyingi kwa mhisani mkuu wa mradi huu, Shirika la Maendeleo la Norway yaani NORAD kwa msaada wao mkubwa kutuwezesha kufanikisha mikakati ya mradi , warsha hii ikiwa ni mojawapo.


13. Baada ya kusema hayo machache nafurahi kutamka rasmi kuwa **Warsha ya Uimarishaji wa Uhusiano Baina ya wakulima, Watafiti na Washauri wa Wakulima** imefungwa.

ASANTENI NA KARIBUNI TENA NJOMBE.


## KIAMBATANISHO NAMBA 6 a: Wakulima wa Mahindi na Viazi



## KIAMBATANISHO NAMBA 6 b: Wakulima wa Mpunga na Ufugaji



# KIAMBATANISHO NAMBA 6 c: Wakulima wa Mahindi




ANGALIA:

Kete 10 zilizo pelekwa kutoka kwenye tatizo la Mmomonyoko wa udogo kwenda kwenye uharibifu wa mazingira zilisahaulika kujumlishwa kwenye jumla ya kete zilizopelekwa kwenye tatizo la uharibifu wa mazingira.